**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE**

**SHULE YA SEKONDARI ISAPULANO,**
**S.L.P 84,**
**MAKETE**

**30/11/2022.**

**Kum Na.MK/DC/IS/SS/J1/03/VOL.____**

**Ndugu,……………………………………………………………………………………………………**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA 2022 KATIKA SHULE YA SEKONDARI ISAPULANO**

Kichwa cha habari hapo juu cha husika. Napenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2022 katika shule ya sekondari Isapulano iliyoko wilaya ya Makete katika mkoa wa Njombe.

**A. TAREHE YA KURIPOTI SHULENI**

Unatakiwa kuripoti shuleni siku ya jumatatu tarehe 09/01/2023 ukiwa na mzazi/ mlezi wako, pia uwe umekamilisha mahitaji yote ya shule kama ambavyo imeainishwa katika barua hii.

**B. SARE ZA SHULE**

**WAVULANA**

i. Suruali mbili rangi ya kaki na damu ya mzee mshono wa linda
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu (tetron)
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba jozi mbili (visiwe na visigino virefu)
iv. Soksi ndefu za rangi nyeusi jozi mbili
v. Sweta mbili rangi ya blue (zenye mshono wa v-shingoni)
vi. Sweta lenye shingo ndefu (pull neck) kwaajili ya kutanguliza ndani ya shati rangi nyeusi au nyeupe
vii. Begi kwaajili ya kubebea daftari

**WASICHANA**

i. Suruali mbili rangi ya kaki na damu ya mzee mshono wa linda
ii. Sketi mbili mshono wa linda rangi ya kaki na damu ya mzee (kitambaa estem No.1), fundi azingatie maagizo ya shule
iii. Mashati mawili meupe mikono mirefu (tetron)
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kambajozi mbili (visiwe na visigino virefu)
v. Soksi ndefu za rangi nyeupe jozi mbili
vi. Sweta mbili rangi ya blue (zenye mshono wa v-shingoni)
vii. Swetalenyeshingondefu (pull neck) kwaajili ya kutanguliza ndani ya shati rangi nyeusi au nyeupe
viii. Begi kwaajili ya kubebea daftari

**T-SHIRT YA SHULE NA KITAMBULISHO**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na t-shirt ya shule ambayo itaandaliwa na shule kwa gharama ya Tsh. 10,000/= pamoja na kitambulisho kwa gharama ya Tsh. 5,000/=

**C. VIFAA VYA TAALUMA**

i. Madaftari makubwa  Q2, Q3, Q4 na daftari za msomi tisa (9)
ii. Vitabu vya masomo
iii. Kamusi ya kiingereza (English to English)
iv. Vifaa vya kuandikia (biki, penseli, rula, ufutio)
v. Mkebe wenye vifaa vyote
vi. Rimu moja aje nayo wakati wa kuripoti
vii. Mchango wa mashine ya kuchapa na kurudufu Tsh. 20,000/=
viii. File moja

**D. VIFAA VYA MICHEZO**

i. Truck suit rangi light blue
ii. Raba za michezo

**E. MCHANGO WA CHAKULA**

Mwanafunzi aje na mchango wa chakula Tsh. 111,000/=, aidha unaweza kutoa kwa awamu mbili kwa Tsh. 55,500/= mwanzo ni mwa muhula wa kwanza yaani Januari na mwanzoni mwa muhula wa pili yaani Julai mara tu shule itakapofunguliwa.

**F. MICHANGO MINGINE**

Aje navyo siku ya kuripoti

i. Jembe lenye mpini
ii. Ndoo lita kumi
iii. Ufagio (chelewa)

**G. FOMU YA KUJAZA NA KUWASILISHA SHULENI SIKU YA KURIPOTI**

i. Medical examination form ambayo imejazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara tu utakapo ripoti shuleni.
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
iii. Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni na maelezo mengine yaliyotolewa/yatakayotolewa na shule.

**KARIBU SANA: "ELIMU NI UKOMBOZI"**

**…………………………………………………**

**LESSA TEOPHIL NSOBHA**


**MAWASILIANO**

**Mkuuwashule: 0767379773**

**Makamu: 0753544288**

# SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na. 25 ya mwaka 1978nakamailivyorekebishwakwasheria Na. 10 yamwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kizingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katka kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na taratibu ya shuleni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (self preparation)
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote wa maisha yako uwapo shuleni
h) Kuzingatiaratibayashulewakatiwote
i) Kutunza mali za umma na
j) Kuongea lugha ya kiingereza muda wote uwapo shuleni

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

a) Kumiliki/kuwa na simu ya mkononi
b) Wizi
c) Uasherati na ushoga
d) Ubakaji
e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
f) Kupigana au kupiga
g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
h) Kudharau bendera ya Taifa
i) Kupata mimba au kusababisha mimba
j) Kuoa au kuolewa
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama washule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kutohudhuria darasani

# SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

KwaMzazi/Mleziwa___________________________________________

1. Napenda kukupongeza kwa mwanao kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2021katikashuleyasekondariIsapulano. Ni mategemeo ya shule kuwa utajitahidi kwa uwezo wako wote kumsaidia ili aweze kusoma bila matatizo kwa kumtimizia mahitaji yote ya muhimu
2. Ili mtoto wako aweze kufanikiwa ni muhimu awepo darasani muda wote wa masomo. Hivyohunabudikumsaidiailivikwazovisivyovyalazimavisiwepo
3. Tafadhali jaza fomu iliyoambatanishwa kama inavyoeleza

## A. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi…………………………………………………………………………………………………………………… Mzazi/Mlezi wa ……..…………………………………………………………..……………………(jina la mtoto) ninakubali mwanangu aje shule ya sekondari Isapulano na ninaahidi kumtimizia mahitaji yote yaliyoagizwa. Pia na ahidi kuwa nitashilikiana na uongozi wa shule kumlea na kumtunza kwa maadili ya ki-Tanzania awapo shuleni na wakati wa likizo mpaka atakapohitimu masomo yake. ***Aidha sitampa au kumruhusu mwanangu kutumia simu awapo shuleni.***

Na kama kuna mabadiliko nita utaarifu uongozi wa shule

Anuani yangu ya kudumu …………………………………………

Namba ya simu…………………………………………………………….

Sahihi…………………………………… Tarehe……………………………………………………..

## B. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi………………………………………………….. Nakubali/Sikubali nafasi niliyopewa katika shule ya Sekondari Isapulano

Naahidi kuwa nitazitii sheria zote za shule nakufuata maelekezo na maagizo nitakayopewa na mkuu wa shule, walimu, wafanyakazi wote na viongozi wote wa serikali ya wanafunzi.

Nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, elimu ya kujitegemea, michezo na kutunza usafi wa mazingira ya shule kwa muda wote nitakaokuwa Isapulano. ***Aidha sitakuwa na simu muda wote niwapo shuleni.***

Shule ya msingi niliyosoma ni……………………………………………………..………………………….

Namba ya mtihani ni………………………………………………………………………………………….

Sahihi …………………………………………………. Tarehe ……………………………………………

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**MAKETE DISTRICT COUNCIL**
**ISAPULANO SECONDARY SCHOOL**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

This form must be completed by government medical officer
Name of student ……………………………………………………………….

Age…………………………………………… Sex……………………………………….

The above named student has been examined in respect of

a) **PREGNANCY TEST (FOR GIRLS ONLY)**
b) **STOOL ……………………………………………………………………………………………………….**
c) **URINE ………………………………………………………………………………………………………..**
d) **CHEST ………………………………………………………………………………………………………**
e) **BLOOD ……………………………………………………………………………………………………….**
f) **EYES ………………………………………………………………………………………………………**
g) **EARS ……………………………………………………………………………………………………….**
h) **OTHER FINDINGS ……………………………………………………………………………….**
**……………………………………………………………………………………………**
**……………………………………………………………………………………………**

I am satisfied that the above named student is fit/Not fit for pursuing secondary studies at Isapulano secondary school

………………………………………  ………………………………………
**SIGNATURE**  **DATE**

…………………………………………………………….  ………………………………………
**DESIGNATION AND OFFICIAL STAMP**  **STATION**